المجلس الأعلى للشئون الإسلامية بتنزانيا
BARAZA KUU LA WAISLAM TANZANIA ( BAKWATA )
THE NATIONAL MUSLIM COUNCIL OF TANZANIA

# KANUNI
# ZA
# JUMUIYA YA WANAWAKE WA KIISLAMU TANZANIA (JUWAKITA-BAKWATA)

S.L.P 21422 DAR ES SALAAM

**TOLEO LA KWANZA MWAKA 2024**

## YALIYOMO


UTANGULIZI ........................................................................................................1

SEHEMU YA KWANZA: TAARIFA YA AWALI YA KANUNI ....................................3

1. JINA LA KANUNI..............................................................................................3

2: TAREHE YA KUANZA KUTUMIKA .....................................................................3

3: MATUMIZI YA KANUNI ......................................................................................3

4: TAFSIRI YA MANENO..........................................................................................3

SEHEMU YA PILI: JINA, MAKAO MAKUU NA NEMBO YA JUWAKITA ..................5

5: JINA LA JUMUIYA ..............................................................................................5

6: MAKAO MAKUU YA JUMUIYA ...........................................................................5

7: NEMBO YA JUMUIYA ..........................................................................................5

SEHEMU YA TATU: MADHUMUNI YA JUWAKITA-BAKWATA ...............................6

8: MADHUMUNI.......................................................................................................6

SEHEMU YA NNE: UANAJUMUIYA, HAKI NA WAJIBU ............................................7

9: SIFA ZA MWANAJUMUIYA...................................................................................7

10: HAKI ZA MWANAJUMUIYA .................................................................................7

11: WAJIBU WA MWANAJUMUIYA.............................................................................7

SEHEMU YA TANO: MUUNDO WA UONGOZI NA VIONGOZI WA JUWAKITA.......9

12: MUUNDO WA UONGOZI .....................................................................................9

13: SIFA ZA KIONGOZI...............................................................................................9

14: KAMATI KUU........................................................................................................9

15: MAJUKUMU YA KAMATI KUU...........................................................................10

16: MAJUKUMU YA VIONGOZI................................................................................10

17: MIIKO YA UONGOZI ..........................................................................................12

18: MUDA WA KUKAA MADARAKANI .....................................................................12

19: UKOMO WA UONGOZI .......................................................................................12

SEHEMU YA SITA: MIKUTANO YA JUWAKITA ........................................................13
20: VIKAO NA MIKUTANO .................................................................................13
21: MIKUTANO YA TAWI ...................................................................................13
22: WAJUMBE WA MKUTANO MKUU WA TAWI ...............................................13
23: MKUTANO MKUU WA MWAKA WA TAWI ...................................................14
24: MAMLAKA YA MKUTANO MKUU WA MWAKA WA TAWI ............................14
25: MKUTANO MKUU WA KAWAIDA WA TAWI ...............................................14
26: MKUTANO MKUU WA DHARURA WA TAWI ...............................................14
27: MIKUTANO YA KATA ....................................................................................15
28: WAJUMBE WA MKUTANO MKUU WA KATA ...............................................15
29: MKUTANO MKUU WA MWAKA WA KATA ...................................................15
30: MAMLAKA YA MKUTANO MKUU WA KATA ................................................15
31: MKUTANO MKUU WA KAWAIDA WA KATA ................................................16
32: MKUTANO MKUU WA DHARURA WA KATA ...............................................16
33: MIKUTANO YA JUWAKITA WILAYA ...........................................................16
34: WAJUMBE WA MKUTANO MKUU WA WILAYA ..........................................17
35: MKUTANO MKUU WA MWAKA WA WILAYA ..............................................17
36: MAMLAKA YA MKUTANO MKUU WA WILAYA ...........................................17
37: MKUTANO MKUU WA KAWAIDA WA WILAYA ...........................................18
38: MKUTANO MKUU WA DHARURA WA WILAYA ..........................................18
39: MIKUTANO YA JUWAKITA MKOA ..............................................................18
40: WAJUMBE WA MKUTANO MKUU WA MKOA ...............................................19
41: MKUTANO MKUU WA MWAKA WA MKOA ...................................................19
42: MAMLAKA YA MKUTANO MKUU WA MWAKA WA MKOA ............................19
43: MKUTANO MKUU WA KAWAIDA WA MKOA ................................................19
44: MKUTANO MKUU WA DHARURA WA MKOA ...............................................20

45: MIKUTANO YA JUWAKITA TAIFA........................................................................20
46: WAJUMBE WA MKUTANO MKUU WA JUWAKITA TAIFA ................................20
47: MKUTANO MKUU WA MWAKA WA JUWAKITA TAIFA...................................21
48: KAZI ZA MKUTANO MKUU WA MWAKA- JUWAKITA TAIFA ..........................21
49: MKUTANO MKUU WA KAWAIDA WA JUWAKITA TAIFA ................................21
50: MKUTANO MKUU WA DHARURA WA JUWAKITA TAIFA ...............................22
51: WAJUMBE WA KAMATI KUU YA JUWAKITA.....................................................22
52: KUTOHUDHURIA MIKUTANO /VIKAO ...............................................................22
SEHEMU YA SABA: UTEUZI NA UCHAGUZI WA VIONGOZI WA JUWAKITA ......23
53: UTEUZI NA UCHAGUZI WA VIONGOZI...............................................................23
54: KUSHIKILIA NAFASI ZILIZOWAZI........................................................................24
55: KUKASIMU MADARAKA KWA UONGOZI .........................................................24
56: KUONDOLEWA KIONGOZI MADARAKANI .......................................................24
SEHEMU YA NANE: VYANZO VYA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ...........26
57: VYANZO VYA MAPATO...........................................................................................26
58: KUPITISHA MAOMBI YA FEDHA ............................................................................26
59: KUTOPITISHA MAOMBI YA FEDHA.......................................................................27
60: KUFUNGUA AKAUNTI YA JUMUIYA.....................................................................27
61: UKAGUZI WA FEDHA ...............................................................................................28
SEHEMU YA TISA:UTATUZI WA MIGOGORO NA MABADILIKO YA KANUNI ....29
62: UTARATIBU WA KUTATUA MIGOGORO ...............................................................29
63: MASUALA YA DINI ......................................................................................................29
64: ITHIBATI YA KANUNI ................................................................................................29

## UTANGULIZI

Wanawake wa Kiislamu wa Baraza Kuu la Waislam wa Tanzania-BAKWATA tunaamini kama Waislamu wengine wote Ulimwenguni, kwamba hakuna apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah peke yake, na kwamba Muhammad (S.A.W) ni Mtume wake wa mwisho hapana tena Mtume baada yake.

Kwa kuwa Qur'an na Sunnah ndiyo mwongozo na ndiyo vitu viwili vikubwa ambavyo Mtume Muhammad (S.A.W) ameviacha kwa Umma wake na sisi lazima tusome Qur'an na hadithi sahihi za Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake na kisha tuzifuate kwa vitendo kwa kutarajia radhi za Allah aliyetakasika.

Tunaamini na tunakubali, kwamba ni wajibu wetu kuendeleza na kuimarisha ITIKADI yetu, na kwamba kuna haja kubwa ya kukuza na kuimarisha ushirikiano, umoja na udugu miongoni mwa Waislamu nchini, kwa hivyo basi kwa Mujibu wa Katiba ya BAKWATA na Miongozo yake, tumeamua kuunda JUMUIYA YA WANAWAKE WA KIISLAMU TANZANIA (JUWAKITA-BAKWATA) kwa lengo la kuratibu, kusimamia na kuongoza shughuli za Wanawake katika mambo mbalimbali ya Wanawake yahusuyo Uislamu, ikiwa pamoja na Nyanja za Ibada, Elimu, Uchumi, Mazingira, Michezo, Ushirikiano na uhusiano na Taasisi za Wanawake wa Kiislamu ndani na nje ya nchi n.k, yenye kuendana na mila na desturi za Kiislamu.

Kuunganisha Wanawake wa kiislamu kwa kufanya Makongamano, Semina za kielimu na mafunzo mbalimbali kwa lengo la kuwajengea uwezo na uelewa katika kuisimamia na kuiendeleza dini yao na Malezi ya familia zao.

Kanuni hizi zimetungwa ili kusaidia na kurahisisha uendeshaji wa Jumuiya ya Wanawake wa Kiislamu Tanzania (JUWAKITA-BAKWATA). Aidha, kanuni hizi zitatumika kuongoza shughuli za kila siku za JUWAKITA-BAKWATA. Endapo itatokea kipengele chochote cha kanuni hizi kimekinzana na Katiba ya BAKWATA, basi Katiba ndio itakayotawala. Wanajumuiya wote wa JUWAKITA-BAKWATA wanawajibika kuzisoma, kuzifahamu, kuziheshimu na kuzitumia kanuni hizi ili kufanikisha uendeshaji mzuri na endelevu wa Jumuiya.

**SEHEMU YA KWANZA**

**TAARIFA YA AWALI YA KANUNI**

## 1. JINA LA KANUNI

Kanuni hizi zitaitwa KANUNI ZA JUMUIYA YA WANAWAKE WA KIISLAMU TANZANIA-BAKWATA ambapo kwa kifupi itajulikana kama KANUNI ZA JUWAKITA-BAKWATA

## 2. TAREHE YA KUANZA KUTUMIKA

Kanuni hizi zimeanza kutumika baada ya kuwasilishwa na kupitishwa na Halmashauri Kuu ya BAKWATA Taifa chini ya Mwenyekiti wake tarehe 18/09/2025.

## 3. MATUMIZI YA KANUNI

Kanuni hizi zitatumiwa na wanajumuiya wa JUWAKITA-BAKWATA Tanzania Bara. Kanuni hizi zitaanza kutumika baada ya kuwasilishwa na kupitishwa na Halmashauri Kuu ya BAKWATA Taifa. Na ikitokea jambo lolote ambalo halipo kwenye Katiba na Kanuni kitaitishwa kikao ili kutafuta ufumbuzi wa jambo hilo.

## 4. TAFSIRI YA MANENO

Katika kanuni hizi baadhi ya maneno yametumika na yana maana yaliyotajwa hapa chini:

i. BAKWATA-Ni Baraza Kuu la Waislam wa Tanzania

ii. DAAWAH-Ni kulingania watu katika dini ya Allah

iii. KAMATI KUU-Ni chombo kinachofanya maamuzi na uratibu wa JUWAKITA-BAKWATA

iv. MAADILI-Ni mwenendo mwema wa viongozi na wanajumuiya wa JUWAIKA-BAKWATA

v. MWANAJUMUIYA-Ni Mwanamke wa Kiislamu aliyesajiliwa JUWAKITA-BAKWATA

vi. SUNNAH-Ni mafundisho na maelekezo ya Mtume Muhammad (Rehema na amani ziwe juu yake).

vii. TAWI – Ni Msikiti wenye wanajumuiya wa JUWAKITA –BAKWATA

viii. VIONGOZI WA JUWAKITA-Ni Mwenyekiti, Katibu, Mweka Hazina na wote walioko katika mlolongo wa Uongozi kwa Mujibu wa Kanuni hizi,

## SEHEMU YA PILI

## JINA, MAKAO MAKUU NA NEMBO YA JUWAKITA

**5. JINA LA JUMUIYA**

Jina la Jumuiya litakuwa: JUMUIYA YA WANAWAKE WA KIISLAMU TANZANIA-BAKWATA na kwa kifupi litajulikana kama JUWAKITA-BAKWATA

**6. MAKAO MAKUU YA JUWAKITA – BAKWATA**

Makao Makuu ya JUWAKITA-BAKWATA Taifa yatakuwa Wilaya ya Kinondoni Mkoa wa Dar es salaam, mahali yalipo Makao Makuu ya BAKWATA Taifa au itakavyoamuliwa vingine.

**7. NEMBO YA JUMUIYA**

Nembo ya JUWAKITA-BAKWATA itakuwa ni alama ya Msikiti, ramani ya Tanzania, Mwezi na nyota.

## SEHEMU YA TATU

## MADHUMUNI YA JUWAKITA-BAKWATA

### 8. MADHUMUNI

JUWAKITA-BAKWATA itakuwa na madhumuni na majukumu yafuatayo:-

a) Kuwaunganisha Wanawake wote wa kiislamu wa Tanzania bara kwa lengo la kuratibu na kusimamia shughuli zote za Dini zinazowahusu Wanawake

b) Kujenga na kudumisha AMANI kwa kutambua kwamba wakati wowote panapokosekana AMANI jamii nzima, hasa wanawake na watoto ndio waathirika wa wakuu.

c) Kulinda, kukuza na kuendeleza heshima, haki na hadhi ya mwanamke kama ilivyoainishwa ndani ya Qur'an na kusisitizwa na Mtume (S.A.W) katika misingi sahihi ya Dini.

d) Kujenga ushirikiano kati ya JUWAKITA-BAKWATA na Jumuiya nyingine zenye kujali Utu, Hadhi na Thamani ya Mwanamke na kuwajengea uwezo wa kutambua thamani yao.

e) Kuratibu na kusimamia ushiriki wa Wanawake kwenye sikukuu za Eid, Maulid, Mwaka Mpya wa Kiislamu na mambo mengine yanayowahusu Wanawake

f) Kufanya Makongamano ya wanawake yenye lengo la kuwaelimisha na kuwajengea uwezo kwenye mambo mbalimbali yanayohusu Dini na Dunia yao

g) Kuratibu na kuhamasisha uwepo wa Madarasa ya Kielimu kwa wanawake ili waifahamu dini yao na kuifuata barabara

h) Kubuni na kuanzisha miradi ya kiuchumi ili kutokomeza umaskini.

i) Kuanzisha vituo vya huduma za kijamii ikiwemo elimu na Afya.

j) Kutoa mafunzo kuhusu maadili sahihi yanayoendana na Uislam kwa vijana na watu wa rika zote kupitia shule, vyuo na majukwaa mbali mbali.

## SEHEMU YA NNE

### UANAJUMUIYA, HAKI NA WAJIBU

**9. SIFA ZA MWANAJUMUIYA**

Kila Mwanamke wa Kiislamu ambaye ni madhehebu ya Sunnat wal Jamaa anaweza kuwa mwanajumuiya wa JUWAKITA-BAKWATA ikiwa ni:-

a) Muislamu Mwanamke mwenye akili timamu
b) Mwenye umri kuanzia miaka 18 na kuendelea
c) Awe ana dumisha utamaduni wa Kiislamu kwa vitendo kama Ibada, Stara nk
d) Awe yuko tayari kujitolea katika shughuli za Kiislamu kwa hali na mali
e) Awe anaguswa na yanayowasibu Waislamu

**10. HAKI ZA MWANAJUMUIYA**

a. Atakuwa na haki ya kuchagua au kuchaguliwa kuwa kiongozi wa JUWAKITA-BAKWATA
b. Atakuwa na haki ya kushiriki shughuli zote za JUWAKITA-BAKWATA
c. Atakuwa na haki ya kujitetea na kutoa maelezo yake mbele ya vikao vya maamuzi endapo kuna mashitaka yaliyotolewa dhidi yake
d. Atakuwa na haki ya kushiriki katika chaguzi za JUWAKITA-BAKWATA

**11. WAJIBU WA MWANAJUMUIYA**

Mwanajumuiya wa JUWAKITA atakuwa na Wajibu ufuatao:-

a. Kupigania Usawa, Haki na Maendeleo ya Wanawake wa Kiislamu hapa nchini

b. Kujielimisha na kujiendeleza kwa faida yake na kwa faida ya Umma kwa ujumla

c. Kushirikiana kwa dhati na wanawake wenzie katika kutoa Elimu kwa jamii

d. Kushiriki katika shughuli zote za JUWAKITA-BAKWATA

e. Kuwa tayari kujikosoa na kukosolewa kwa hekima kwa maslahi ya JUWAKITA-BAKWATA

## SEHEMU YA TANO
## MUUNDO WA UONGOZI NA VIONGOZI WA JUWAKITA

### 12. MUUNDO WA UONGOZI

Uongozi wa JUWAKITA-BAKWATA utakuwa kama ifuatavyo

a. Kamati Kuu
b. Mkutano Mkuu
c. Kamati za JUWAKITA-BAKWATA

### 13. SIFA ZA KIONGOZI

Kiongozi yeyote wa JUWAKITA-BAKWATA sharti awe Muislamu, pamoja na kutimiza masharti ya Uanajumuiya kama ilivyoelezwa kwenye kanuni hizi, Kiongozi wa Jumuiya sharti awe na sifa zifuatazo: -

a. Awe Muislamu mwenye akili timamu, na awe anao ufahamu juu ya Uislamu
b. Awe mwenye shughuli halali inayomwingizia kipato kama vile mkulima, mfanyabiashara, mfanyakazi au mfugaji nk.
c. Awe muadilifu, muaminifu, mkweli kwa JUWAKITA-BAKWATA na anaikubali na kuifuata Katiba ya BAKWATA
d. Awe anayekubali kujisahihisha, kusahihishwa ikiwa hapana budi akubali kuwajibika kwa maslahi ya Umma

### 14. KAMATI KUU

Kutakuwa na kamati kuu ya JUWAKITA-BAKWATA. Kamati kuu itaundwa na wajumbe wafuatao:

a) Mwenyekiti
b) Makamu Mwenyekiti
c) Katibu
d) Naibu katibu
e) Mweka Hazina
f) Wajumbe watano wenye majukumu maalum
g) Walezi wa Kanda

## 15. MAJUKUMU YA KAMATI KUU

a) Kusimamia utendaji kazi za kila siku katika ofisi za JUWAKITA-BAKWATA
b) Kupokea na kutekeleza maamuzi na maelekezo/ maagizo ya BAKWATA-BAKWATA
c) Kusimamia na kuratibu vikao na Mikutano
d) Kuandaa taarifa ya mapato na matumizi ya Jumuiya ya mwaka uliopita na kuiwasilisha kwenye Mkutano Mkuu
e) Kuandaa bajeti ya mapato na matumizi ya kila mwaka na kuiwasilisha kwenye Mkutano Mkuu
f) Kuandaa taarifa ya utendaji kazi za Jumuiya na kuziwasilisha kwenye Mkutano Mkuu
g) Kuandaa Mpango Mkatati wa miaka mitano
h) Kusimamia Utekelezaji wa Mpango Mkakati na Kuanda mpango kazi wa kila mwaka
i) Kuandaa taarifa za utekelezaji wa mpango mkakati na kuwasilisha kwa Katibu Mkuu wa BAKWATA

## 16. MAJUKUMU YA VIONGOZI

Viongozi wa Jumuiya hii watakuwa na majukumu yafuatayo:

### I. Mwenyekiti

a) Atakuwa ndiye kiongozi na msimamizi mkuu wa shughuli zote za JUWAKITA-BAKWATA.

b) Atasimamia mikutano na vikao vyote vya jumuiya ngazi ya Taifa.

c) Atahakikisha viongozi wengine wote wanawajibika ipasavyo.

### II. Makamu Mwenyekiti

a) Atakuwa ndiye msaidizi mkuu wa Mwenyekiti.

b) Atafanya majukumu ya Mwenyekiti pale asipokuepo.

c) Atafanya kazi yoyote atakayoelekezwa na Mwenyekiti.

**III. Katibu**

a) Atakuwa ndiye Mtendaji Mkuu wa jumuiya hii.

b) Ataandaa mikutano/vikao na agenda za mikutano/vikao kwa kushirikiana na Mwenyekiti.

c) Atakuwa mwandishi wa Muhtasari wa mikutano na vikao vyote vya Jumuiya

d) Ataandaa, kutuma na kupokea na kuhifadhi mawasiliano yote ya Jumuiya.

e) Atakuwa ndiye mdhibiti na mtunza siri na nyaraka mbalimbali za Jumuiya

**IV. Naibu Katibu**

a) Atakuwa ndiye Msaidizi Mkuu wa Katibu.

b) Atafanya majukumu ya Katibu pale anapokuwa hayupo.

c) Atafanya kazi yoyote kwa maelekezo ya Katibu.

**V. Mweka Hazina**

a) Atakuwa mtunza fedha za Jumuiya hii.

b) Atawajibika kuandaa na kutoa taarifa za fedha za Jumuiya kwa kila mwezi na pale inapohitajika.

c) Atahusika kulipa malipo yote yaliyoidhinishwa kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa.

d) Atawajibika kuandaa ripoti ya fedha ya mapato na matumizi.

## 17. MIIKO YA UONGOZI

a. Ni mwiko kwa kiongozi wa JUWAKITA-BAKWATA kutumia Madaraka aliyopewa na waislamu kwa ajili ya manufaa yake binafsi au kwa upendeleo au kwa maana yoyote ambayo ni kinyume na lengo lililokusudiwa na madaraka hayo.

b. Ni mwiko Kutoa maelezo, taarifa, au siri za JUWAKITA-BAKWATA kwa mtu au chombo chochote bila idhini ya mamlaka inayohusika

c. Ni mwiko Kutoa au kupokea RUSHWA, kushiriki katika shughuli HARAMU kwa mujibu wa dini na mwongozo wa BAKWATA.

## 18. MUDA WA KUKAA MADARAKANI

Kiongozi yeyote wa JUWAKITA-BAKWATA aliyeteuliwa au aliyechaguliwa kwa mujibu wa kanuni hizi atashika madaraka yake kwa muda wa miaka mitano (5) ya kipindi cha uongozi na anaweza kuteuliwa au kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka mitano (5) endapo bado anazo sifa za kuwa kiongozi na hakutokuwa na ukomo wa kukaa madarakani.

## 19. UKOMO WA UONGOZI

a) Kifo
b) Kujiuzulu
c) Kujitoa au kufukuzwa uanachama
d) Kutenguliwa au kuondolewa na Mamlaka
e) Kuritadi (kutoka katika Uislamu)
f) Kurukwa na akili au kuugua ugonjwa ambao utapelekea kushindwa kufanya majukumu yake.

## SEHEMU YA SITA
## MIKUTANO YA JUMUIYA

### 20. VIKAO NA MIKUTANO

JUWAKITA-BAKWATA itakuwa na mikutano na vikao katika kila ngazi. Kikao cha mwanzo cha Jumuiya hii kitakuwa ni tawi. Kwa mujibu wa kanuni hizi ifahamike kuwa Tawi ni MSIKITI wa eneo ambapo Jumuiya inatekeleza Majukumu yao. Kila mwaka kutakuwa na mkutano mkuu wa mwaka mmoja utakaofanyika mwezi Disemba, mkutano mkuu wa kawaida utakaofanyika kila baada ya miezi mitatu, na mkutano mkuu wa dharura utakaofanyika wakati wowote kunapokuwa na jambo la dharura la kujadiliwa.

### 21. MIKUTANO YA TAWI

Kutakuwa na mikutano ya Tawi ya JUWAKITA-BAKWATA kama ifuatavyo:

a) Mkutano mkuu wa mwaka wa Tawi
b) Mkutano mkuu wa kawaida wa Tawi
c) Mkutano mkuu wa dharura wa Tawi

### 22. WAJUMBE WA MKUTANO MKUU WA TAWI

Mkutano mkuu wa tawi wa Jumuiya utakuwa na wajumbe wafuatao:

a) Mwenyekiti wa JUWAKITA-BAKWATA wa tawi
b) Katibu wa JUWAKITA-BAKWATA wa tawi
c) Mweka hazina wa JUWAKITA-BAKWATA wa tawi
d) Wajumbe wote wa kamati ya JUWAKITA wa tawi
e) Waumini wote (wanawake) wanaoishi katika tawi husika
f) Kiongozi yeyote wa JUWAKITA-BAKWATA wa ngazi ya juu anayeishi katika tawi husika
g) Mkutano mkuu wa JUWAKITA-BAKWATA wa tawi ndiyo kikao cha juu cha Masuala yote yanayohusu shughuli za Jumuiya katika tawi kwa mujibu wa Kanuni hii, isipokuwa yale tu ambayo yamewekwa wazi na Katiba ya BAKWATA.

## 23. MKUTANO MKUU WA MWAKA WA TAWI

Kutakuwa na Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Tawi ambao utafanyika mwezi Disemba ya kila mwaka.

## 24. MAMLAKA YA MKUTANO MKUU WA MWAKA WA TAWI

a) Kuchagua viongozi wote wa tawi kama:
   - i. Mwenyekiti wa JUWAKITA-BAKWATA wa Tawi
   - ii. Katibu wa JUWAKITA-BAKWATA wa Tawi
   - iii. Mweka hazina wa JUWAKITA-BAKWATA wa Tawi
   - iv. Wajumbe wawili (2) wa Mkutano Mkuu wa Kata wanaowakilisha tawi
   - v. Wajumbe watano (5) wa Kamati ya Tawi

b) Kumsimamisha Uongozi kiongozi yoyote wa JUWAKITA-BAKWATA wa tawi endapo imedhihirika kuwa tabia na matendo yake hayaendani na Qur'an na Sunnah wala na Maadili ya BAKWATA.

## 25. MKUTANO MKUU WA KAWAIDA WA TAWI

a) Kutakuwa na Mkutano wa Kawaida wa Tawi ambao utahudhuriwa na wajumbe waliotajwa kwenye Mkutano Mkuu kujadili maendeleo ya Jumuiya kwa kipindi cha miezi mitatu.

b) Mkutano huu utafanyika kila baada ya miezi mitatu (3) tokea tarehe ya Mkutano Mkuu wa Mwaka kufanyika.

## 26. MKUTANO MKUU WA DHARURA WA TAWI

a) Kutakuwa na Mkutano wa Dharura wa Tawi utakaoitishwa wakati wowote kunapokuwa na jambo la kujadiliwa kwa dharura.

b) Mkutano huu utahudhuriwa na wajumbe wa Mkutano

Mkuu kujadili jambo muhimu la dharura tu, ambalo haliwezi kusubiri Mkutano Mkuu wa Mwaka au ule wa Kawaida.

## 27. MIKUTANO YA KATA

Kutakuwa na Mikutano ya Kata kama ifuatavyo:-

a) Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Kata
b) Mkutano Mkuu wa Kawaida wa Kata
c) Mkutano Mkuu wa Dharura wa Kata

## 28. WAJUMBE WA MKUTANO MKUU WA KATA

Mkutano Mkuu wa Kata ndiyo kikao chenye kauli ya mwisho juu ya masuala yote yanayohusu shughuli za JUWAKITA-BAKWATA katika Kata kwa mujibu wa kanuni hii, isipokuwa yale tu ambayo Katiba ya BAKWATA imeyaweka wazi kuwa yatashughulikiwa na Baraza. Wajumbe wa Mkutano huu ni:

a. Mwenyekiti wa JUWAKITA-BAKWATA wa Kata
b. Katibu wa JUWAKITA-BAKWATA wa Kata
c. Mweka hazina wa JUWAKITA-BAKWATA wa Kata
d. Wajumbe wawili (2) waliochaguliwa kutoka kila tawi waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa Tawi
e. Viongozi wote wa Vikao vya juu vya JUWAKITA-BAKWATA wanaoishi katika Kata hiyo

## 29. MKUTANO MKUU WA MWAKA WA KATA

Kutakuwa na Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Kata ambao utafanyika mwezi Disemba ya kila mwaka.

## 30. MAMLAKA YA MKUTANO MKUU WA MWAKA WA KATA

Kutakuwa na Mkutano mkuu wa Kata utakakuwa na Mamlaka yafuatayo: -

a. Kujadili shughuli za maendeleo ya JUWAKITA-BAKWATA kwenye Kata kwa mwaka.

b. Kuchagua Viongozi wa Jumuiya katika Kata ambao ni:
   i. Mwenyekiti wa JUWAKITA-BAKWATA wa Kata
   ii. Katibu wa JUWAKITA-BAKWATA wa Kata
   iii. Mweka hazina wa JUWAKITA-BAKWATA wa Kata
   iv. Wajumbe wawili (2) wa Mkutano Mkuu wa Wilaya

c. Kupitia, kujadili na kutolea maamuzi malalamiko au maazimio toka vikao vya chini

**31. MKUTANO MKUU WA KAWAIDA WA KATA**

a) Kutakuwa na Mkutano wa Kawaida wa Kata ambao utahudhuriwa na wajumbe waliotajwa kwenye Mkutano Mkuu kujadili maendeleo ya Jumuiya kwa kipindi cha miezi mitatu.

b) Mkutano huu utafanyika kila baada ya miezi mitatu (3) tokea tarehe ya Mkutano Mkuu wa Mwaka kufanyika.

**32. MKUTANO MKUU WA DHARURA WA KATA**

a) Kutakuwa na Mkutano wa Dharura wa Kata utakaoitishwa wakati wowote kunapokuwa na jambo la kujadiliwa kwa dharura.

b) Mkutano huu utahudhuriwa na wajumbe wa Mkutano Mkuu kujadili jambo muhimu la dharura tu, ambalo haliwezi kusubiri Mkutano Mkuu wa Mwaka au ule wa Kawaida.

**33. MIKUTANO YA JUWAKITA WILAYA**

Katika ngazi ya Wilaya JUWAKITA itakuwa na vikao vifuatavyo:-

i. Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Wilaya
ii. Mkutano Mkuu wa Kawaida wa Wilaya
iii. Mkutano Mkuu wa Dharura wa Wilaya

### 34. WAJUMBE WA MKUTANO MKUU WA WILAYA

Mkutano mkuu wa wilaya ndiyo kikao chenye kauli ya mwisho kwa mujibu wa kanuni hizi juu ya shughuli zote za JUWAKITA-BAKWATA, isipokuwa yale ambayo Katiba ya BAKWATA imeeleza vinginevyo. Mkutano mkuu wa Wilaya utakaokuwa na wajumbe wafuatao: -

a. Mwenyekiti wa JUWAKITA-BAKWATA wa Wilaya
b. Katibu wa Wilaya wa JUWAKITA-BAKWATA wa Wilaya
c. Wenyeviti wote wa JUWAKITA-BAKWATA wa Kata
d. Makatibu wote wa JUWAKITA-BAKWATA wa Kata
e. Wajumbe wawili wa Mkutano Mkuu wa Wilaya kutoka kila Kata ya Wilaya
f. Wajumbe wa vikao vya juu wa JUWAKITA-BAKWATA wanaoishi katika wilaya hiyo

### 35. MKUTANO MKUU WA MWAKA WA WILAYA

Kutakuwa na Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Wilaya ambao utafanyika mwezi Disemba ya kila mwaka.

### 36. MAMLAKA YA MKUTANO MKUU WA MWAKA WA WILAYA

Mkutano Mkuu wa JUWAKITA Wilaya ndiyo kikao chenye kauli ya mwisho katika wilaya husika kwa mujibu wa Kanuni hizi, labda pale ambapo imeeleza vinginevyo kwenye Katiba ya BAKWATA. Mkutano Mkuu wa Wilaya utakuwa na mamlaka yafuatayo:-

a. Kuchagua Mwenyekiti wa JUWAKITA-BAKWATA wa Wilaya
b. Kupokea uteuzi wa Katibu wa JUWAKITA-BAKWATA wa Wilaya
c. Kuajiri Mweka hazina/Mhasibu wa Jumuiya wa Wilaya
d. Kuchagua wajumbe wawili (2) watakao wakilisha Mkutano Mkuu wa Mkoa kutoka wilaya
e. Kuchagua wajumbe saba (7) wa Kamati ya JUWAKITA-BAKWATA wa Wilaya
f. Kujadili na kupanga shughuli za JUWAKITA-BAKWATA kwenye Wilaya

g. Kufanya Tathimini ya Mipango ya shughuli za JUWAKITA-BAKWATA katika wilaya

h. Kupokea na kuidhinisha Makisio ya Mapato na Matumizi ya Wilaya mwaka hadi mwaka

i. Kumsimamisha, Kumfukuza Kiongozi yoyote wa JUWAKITA-BAKWATA ngazi ya Wilaya itakapodhihirika kuwa matendo yake na tabia yake hayaendani na Qur'an na Sunnah

## 37. MKUTANO MKUU WA KAWAIDA WA WILAYA

a) Kutakuwa na Mkutano wa Kawaida wa Wilaya ambao utahudhuriwa na wajumbe waliotajwa kwenye Mkutano Mkuu kujadili maendeleo ya Jumuiya kwa kipindi cha miezi mitatu.

b) Mkutano huu utafanyika kila baada ya miezi mitatu (3) tokea tarehe ya Mkutano Mkuu wa Mwaka kufanyika.

## 38. MKUTANO MKUU WA DHARURA WA WILAYA

a) Kutakuwa na Mkutano wa Dharura wa Wilaya utakaoitishwa wakati wowote kunapokuwa na jambo la kujadiliwa kwa dharura.

b) Mkutano huu utahudhuriwa na wajumbe wa Mkutano Mkuu kujadili jambo muhimu la dharura tu, ambalo haliwezi kusubiri Mkutano Mkuu wa Mwaka au ule wa Kawaida.

## 39. MIKUTANO YA JUWAKITA-BAKWATA MKOA

Katika ngazi ya Mkoa Jumuiya itakuwa na Mikutano ifuatayo:-

a) Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Mkoa

b) Mkutano Mkuu wa Kawaida wa Mkoa

c) Mkutano Mkuu wa dharura wa Mkoa

**40. WAJUMBE WA MKUTANO MKUU WA MKOA**

i. Mwenyekiti wa JUWAKITA-BAKWATA wa Mkoa
ii. Katibu wa JUWAKITA-BAKWATA wa Mkoa
iii. Mweka hazina wa JUWAKITA-BAKWATA wa Mkoa
iv. Wajumbe wawili toka kila Wilaya ya mkoa huo
v. Wajumbe wa vikao vya juu wanaoishi katika Mkoa huo
vi. Wenyeviti na Makatibu wote wa Wilaya za Mkoa huo

**41. MKUTANO MKUU WA MWAKA WA MKOA**

Kutakuwa na Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Mkoa ambao utafanyika mwezi Disemba ya kila mwaka.

**42. MAMLAKA YA MKUTANO MKUU WA MWAKA WA MKOA**

a. Kuchagua Mwenyekiti wa JUWAKITA-BAKWATA wa Mkoa
b. Kupokea teuzi za Katibu wa JUWAKITA-BAKWATA wa Mkoa
c. Kuajiri Mweka hazina/ Mhasibu wa Jumuiya wa Mkoa
d. Kutekeleza mpango mkakati wa miaka mitano wa Jumuiya, kuandaa mpango kazi wa kila mwaka wa Mkoa na kuandaa taarifa za utekelezaji za mpangokazi huo.
e. Kuwachagua wajumbe kumi (10) watakaoingia kwenye Kamati kuu ya Mkoa
f. Kuandaa, kupokea na kuidhinisha Makisio ya mapato na matumizi ya mkoa ya kila mwaka
g. Kufanya tathmini ya Mipango ya shughuli za JUWAKITA-BAKWATA kwenye Mkoa
h. Kuwasimamisha Viongozi kwa ngazi ya Mkoa endapo itajiridhisha kuwa matendo na mwenendo wake havilingani na Qur'an na Sunnah wala maadili ya BAKWATA,

**43. MKUTANO MKUU WA KAWAIDA WA MKOA**

a) Kutakuwa na Mkutano wa Kawaida wa Mkoa ambao utahudhuriwa na wajumbe waliotajwa kwenye Mkutano

Mkuu kujadili maendeleo ya Jumuiya kwa kipindi cha miezi mitatu.

b) Mkutano huu utafanyika kila baada ya miezi mitatu (3) tokea tarehe ya Mkutano Mkuu wa Mwaka kufanyika.

**44. MKUTANO MKUU WA DHARURA WA MKOA**

a) Kutakuwa na Mkutano wa Dharura wa Mkoa utakaoitishwa wakati wowote kunapokuwa na jambo la kujadiliwa kwa dharura.

b) Mkutano huu utahudhuriwa na wajumbe wa Mkutano Mkuu kujadili jambo muhimu la dharura tu, ambalo haliwezi kusubiri Mkutano Mkuu wa Mwaka au ule wa Kawaida.

**45. MIKUTANO YA JUWAKITA TAIFA**

Kutakuwa na Mikutano mikuu 3 kama ifuatavyo:-

a. Mkutano Mkuu wa Mwaka
b. Mkutano Mkuu wa Kawaida
c. Mkutano Mkuu wa Dharura

**46. WAJUMBE WA MKUTANO MKUU WA JUWAKITA-BAKWATA TAIFA**

Mkutano Mkuu wa JUWAKITA-BAKWATA wa Taifa utakuwa na wajumbe wafuatao: -

a) Mwenyekiti wa JUWAKITA-BAKWATA Taifa
b) Makamu Mwenyekiti wa JUWAKITA-BAKWATA Taifa
c) Katibu wa JUWAKITA-BAKWATA Taifa
d) Naibu Katibu wa JUWAKITA-BAKWATA Taifa
e) Wajumbe wa Kamati kuu JUWAKITA-BAKWATA Taifa
f) Wajumbe watatu (3) kutoka kila Mkoa
g) Wajumbe kumi (10) walioteuliwa na Mwenyekiti
h) Wenyeviti na makamu wote wa JUWAKITA-BAKWATA Mikoa na Wilaya
i) Makatibu na manaibu wote wa JUWAKITA-BAKWATA Mikoa na Wilaya
j) Waweka Hazina wote wa JUWAKITA-BAKWATA Mkoa na Wilaya

## 47. MKUTANO MKUU WA MWAKA WA JUWAKITA TAIFA

Kutakuwa na Mkutano Mkuu wa Mwaka wa JUWAKITA-BAKWATA Taifa ambao utafanyika mwezi Disemba ya kila mwaka. Mkutano Mkuu wa JUWAKITA-BAKWATA Taifa utakuwa ndicho kikao kikuu kupita vyote vya Jumuiya.

## 48. KAZI ZA MKUTANO MKUU WA MWAKA WA JUWAKITA-BAKWATA TAIFA

a) Kukiagiza kikao chochote cha Jumuiya katika ngazi zote kufanya kazi zozote ambazo Mkutano Mkuu utaona inafaa

b) Kubadili au kuongeza chochote kwenye Kanuni za Jumuiya kwa maelekezo ya Halmashauri kuu Taifa na mamlaka za juu nyingine za BAKWATA Taifa.

c) Utapokea na kujadili taarifa ya kazi za Jumuiya zilizoandaliwa na Kamati Kuu na kutoa maelekezo ya utekelezaji kwa mujibu wa taratibu za BAKWATA zinazohusu Maendeleo ya Wanawake na Mipango ya Jumuiya

d) Kupokea uteuzi wa viongozi wa juu kama vile Mwenyekiti, Mwakamu Mwenyekiti na Katibu wa JUWAKITA-BAKWATA ngazi ya Taifa.

e) Kuajiri Mweka hazina/Mhasibu wa JUWAKITA-BAKWATA Taifa.

f) Kuchagua wajumbe watano (5) wa Kamati Kuu ya JUWAKITA-BAKWATA Taifa

g) Kuteua Walezi wa Kanda wa JUWAKITA-BAKWATA.

## 49. MKUTANO MKUU WA KAWAIDA WA JUWAKITA-BAKWATA TAIFA

a) Kutakuwa na Mkutano wa Kawaida wa JUWAKITA-BAKWATA Taifa ambao utahudhuriwa na wajumbe waliotajwa kwenye Mkutano Mkuu kujadili maendeleo ya Jumuiya kwa kipindi cha miezi mitatu.

b) Mkutano huu utafanyika kila baada ya miezi mitatu (3) tokea tarehe ya Mkutano Mkuu wa Mwaka kufanyika.

## 50. MKUTANO MKUU WA DHARURA WA JUWAKITA-BAKWATA TAIFA

a) Kutakuwa na Mkutano wa Dharura wa Jumuiya Taifa utakaoitishwa wakati wowote kunapokuwa na jambo la kujadiliwa kwa dharura.

b) Mkutano huu utahudhuriwa na wajumbe wa Mkutano Mkuu kujadili jambo muhimu la dharura tu, ambalo haliwezi kusubiri Mkutano Mkuu wa Mwaka au ule wa Kawaida.

## 51. KAMATI KUU YA JUWAKITA-BAKWATA

Kutakuwa na kamati Kuu ya JUWAKITA-BAKWATA. Kamati Kuu inaweza kumwalika Mjumbe yoyote (Mwanamke) kuhudhuria kwenye kikao cha Kamati Kuu endapo itahitajika kufanya hivyo. Wajumbe wa Kamati Kuu ya JUWAKITA-BAKWATA ni hawa wafuatao:

a) Mwenyekiti wa JUWAKITA-BAKWATA Taifa

b) Makamu Mwenyekiti wa JUWAKITA-BAKWATA Taifa

c) Katibu wa JUWAKITA-BAKWATA Taifa

d) Naibu Katibu wa JUWAKITA-BAKWATA Taifa

e) Wajumbe 5 wa Kamati Kuu JUWAKITA-BAKWATA Taifa

f) Walezi wa Kanda wa JUWAKITA-BAKWATA

## 52. KUTOHUDHURIA VIKAO

a. Mwanajumuiya asipofika kwenye vikao bila taarifa atakuwa amefanya kosa ambalo atachukuliwa hatua.

b. Mwanajumuiya asipofika kwenye vikao viwili mfululizo bila taarifa atapewa onyo na mara ya tatu asipohudhuria anaweza kuondolewa uanachama na kufutwa kwenye daftari la uwanajumuiya.

## SEHEMU YA SABA
## UTEUZI NA UCHAGUZI WA VIONGOZI WA JUWAKITA

### 53. UTEUZI NA UCHAGUZI WA VIONGOZI

Kutakuwa na viongozi wa kuteuliwa na kuchaguliwa kwa utaratibu ufuatao:

a) Uteuzi wa viongozi utafanyika kila baada ya miaka mitano (5) baada ya viongozi waliokuwa madarakani kumaliza muda wao.

b) Uteuzi wa Mwenyekiti na Makamu mwenyekiti wa JUWAKITA-BAKWATA Taifa utafanywa na Mufti na Sheikh Mkuu wa Tanzania.

c) Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa JUWAKITA-BAKWATA ngazi za Mkoa na Wilaya watachaguliwa kwa kupigiwa kura na Mkutano mkuu katika ngazi husika.

d) Uteuzi wa Makatibu wa JUWAKITA-BAKWATA Taifa, Mikoa na Wilaya utafanywa na Katibu Mkuu wa BAKWATA.

e) Mweka Hazina (Mhasibu) wa JUWAKITA-BAKWATA katika ngazi Taifa, Mkoa na Wilaya watakuwa ni waajiriwa.

f) Viongozi wote wa JUWAKITA katika Kata na Matawi watachaguliwa na Mkutano Mkuu katika ngazi husika.

g) Uchaguzi utasimamiwa na kamati ya uchaguzi itakayoundwa kwa mujibu wa sheria na kwa kazi hiyo tu. Kamati hiyo itakuwa na Mwenyekiti, katibu na wajumbe watatu.

h) Katika chaguzi za Viongozi, mshindi ni yule atakayepata kura nyingi zaidi.

i) Katika chaguzi, kura zitakazopigwa zitakuwa ni kura za siri

j) Kamati ya uchaguzi ndio chombo kitakachosimamia uchaguzi katika hatua zote na kwamba baada ya kumaliza zoezi la kupiga na kuhesabu kura mshindi atatangazwa katika eneo ambalo uchaguzi umefanyika.

k) Kutakuwa na Mawakala wa kila mgombea wakati wa kuhesabu kura.

l) Uchaguzi wa marudio utafanyika ikiwa wagombea watalingana kwa kura, ikiwa kura zitalingana kwa mara ya pili, mwenyekiti wa JUWAKITA-BAKWATA katika ngazi husika atakuwa na kura ya turufu.

m) Mgombea anaweza kukata rufaa katika ngazi za juu kwa kujaza fomu maalum ndani ya masaa 24 baada ya kutangazwa matokeo.

## 54. KUSHIKILIA NAFASI ZILIZO WAZI

Iwapo nafasi katika wadhifa wowote wa JUWAKITA-BAKWATA itabaki wazi kutokana na moja ya sababu zilizoorodheshwa katika Kanuni hii, iwapo aliyekosekana ni kiongozi basi Naibu atashika nafasi lakini iwapo aliyekosekana ni Naibu basi nafasi hiyo itaendelea kubaki wazi mpaka uteuzi au uchaguzi utakapofanyika.

## 55. KUKASIMU MADARAKA KWA UONGOZI

Endapo Mwenyekiti hatakuwepo, atakasimu madaraka yake kwa Makamu Mwenyekiti na kama wote watakuwa hawapo aidha kwa kujiuzulu au kwa dharura yoyote, atateuliwa Mwenyekiti wa muda kukaimu madaraka hayo. Uteuzi au uchaguzi utafanyika ndani ya siku 90 ili kuziba nafasi hiyo.

## 56. KUONDOLEWA KIONGOZI MADARAKANI

Kiongozi yoyote anaweza kuondolewa madarakani kabla ya muda wake wa uongozi kuisha endapo atapoteza sifa za kuwa kiongozi kwa mujibu wa kanuni hii. Baadhi ya sababu za kiongozi kuondolewa madarakani ni kama zifuatazo:

a) Kubadili dini

b) Kurukwa na akili

c) Kufanya matendo maovu kinyume na mafundisho ya Uislamu.

d) Kutohudhuria mikutano na au vikao vitatu mfululizo bila ya ruhusa maalum.

e) Ubadhirifu wa fedha au wizi wa mali za JUWAKITA-BAKWATA

## SEHEMU YA NANE
## VYANZO VYA MAPATO NA KANUNI ZA FEDHA

### 57. VYANZO VYA MAPATO

a) Michango ya hiari ya wanajumuiya

b) Mapato kutokana na miradi ya Kiuchumi

c) Ruzuku na Misaada kutoka kwa wahisani na wafadhili

### 58. KUPITISHA MAOMBI YA FEDHA

a. Maombi yote ya kuomba fedha yatapitishwa kwa Umakini kwa kuzingatia umuhimu wa fedha inayoombwa.

b. Maombi ya kuomba fedha ya Kutekeleza miradi ya JUWAKITA-BAKWATA itapitishwa kwa umakini mkubwa na kwa uangalifu kabla ya kutumika kwa kusudio la kuomba fedha hizo.

c. Hati ya Maombi ya fedha (Requisition) kwa ajili ya matumizi ya kawaida itajazwa na muombaji ikiambatanishwa na nyaraka halali za kiuhasibu na kuipitisha kwa kiongozi wake wa kamati kwa ajili ya uthibitisho.

d. Hati hiyo itapelekwa kwa Mwenyekiti kwa ajili ya kupata kibali cha matumizi.

e. Muweka Hazina atakagua nyaraka zote kuhakikisha kuwa zipo sawa ndipo atafanya malipo.

f. Muombaji ataitia saini hati ya malipo kabla ya kukabidhiwa pesa.

g. Muombaji ataenda kununua kitu alichokiomba na kukiambatanisha na stakabadhi ya manunuzi kuthibitisha kafanya manunuzi na kuirudisha kwa Mweka Hazina.

h. Mweka Hazina atamsainisha hati ya mapokezi na kuambatanisha risiti na hati ya malipo.

i. Taratibu kama hizo zitafuatwa kwa manunuzi ya mali (Capital goods) isipokuwa Mweka Hazina Mkuu atahakikisha kuwa kinachonunuliwa kipo katika bajeti.
j. Mwenyekiti na kamati yake ya fedha watajadili na kuyapitisha maombi hayo ya fedha baada ya kupitishwa na Mkutano Mkuu.
k. Mweka Hazina atawajibika kutunza taarifa zote za fedha na kuzitolea ufafanuzi atakapotakiwa kufanya hivyo na Mkutano Mkuu, wakaguzi wa hesabu au mkutano wowote.

## 59. KUTOPITISHA MAOMBI YA FEDHA

a) Tahadhari kubwa itachukuliwa katika kupitisha maombi ya fedha ili kudhibiti mianya ya ubadhirifu wa fedha za Jumuiya.
b) Maombi yoyote ya fedha yasiyofuata utaratibu uliowekwa hayatapitishwa au kushughulikiwa.
c) Utaratibu wa kuomba fedha ni sharti ufuatwe ili kujiridhisha na uhalali wa maombi hayo.
d) Mweka Hazina atawajibika kutunza taarifa zote za fedha kuzitolea ufafanuzi atakapotakiwa kufanya hivyo na mkutano mkuu au mkutano wowote au kikao chochote pamoja na ukaguzi.

## 60. KUFUNGUA AKAUNTI ZA JUMUIYA

a) Fedha zote za JUWAKITA zitatunzwa katika Benki kama itakavyo elekezwa na Mkutano Mkuu wa JUWAKITA-BAKWATA Taifa
b) Malipo ya fedha zote yatafanyika kwa kutumia hundi ambazo zitasainiwa kundi A na kundi B ambapo watatokana na viongozi wa juu.
c) Mweka Hazina atatakiwa kutunza fedha na nyaraka nyeti za Taasisi ndani ya Safe.
d) Ufunguo wa safe wa utatunzwa na Mjumbe atakayeteuliwa na Mkutano Mkuu wa JUWAKITA-BAKWATA wa ngazi husika.

e) Mweka Hazina atawajibika kuandaa taarifa za fedha kila mwaka na kutoa taarifa katika Mkutano.

## 61. UKAGUZI WA FEDHA

a. Mkaguzi wa nje wa fedha atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa JUWAKITA-BAKWATA na kufanya kazi kwa uhuru bila kuingiliwa.
b. Mkaguzi wa nje atawajibika kuandaa taarifa za ukaguzi wa fedha na kuziwasilisha kwenye Halmashauri Kuu ya BAKWATA Taifa.
c. Mkaguzi mkuu wa nje ni sharti awe Mhasibu aliyesajiliwa na Bodi ya Wahasibu ya Taifa.
d. Kama kuna miradi inayohusisha wanajumuiya na Mwanajumuiya akahitaji kupewa fedha zake za gawio atajaza fomu maalum ya maombi ya fedha kama ilivyokuwa kwenye kanuni hizi na kuikabidhi kwa Mweka Hazina ili kuandaa malipo.

## SEHEMU YA TISA

## UTATUZI WA MIGOGORO NA MABADILIKO YA KANUNI

### 62. UTARATIBU WA KUTATUA MIGOGORO

Kutakuwa na Kamati ya Maadali itakayoteuliwa na Mkutano Mkuu wa ngazi husika na kuwajibika kwa Kamti kuu ya ngazi hiyo. Kamati ya Maadili itakuwa na wajumbe watatu na itafanya kazi zifuatazo:

(i) Migogoro yote ya kiutendaji au uongozi itashughulikiwa kwa mujibu wa Katiba na Miongozo ya BAKWATA na uamuzi wake utakuwa wa mwisho

(ii) Katika hatua za awali, Kamati ya maadili itasimamia maadili ya viongozi na wanajumuiya pamoja na utatuzi wa migogoro na usuluhishi

(iii) Endapo mgogoro utakuwa mkubwa, shauri hilo litapelekwa katika Kamati kuu na kisha kwenye Mkutano mkuu kwa maamuzi zaidi.

### 63. MASUALA YA DINI

Masuala ya dini katika JUWAKITA-BAKWATA yatasimamiwa na BAKWATA kwa miongozo iliyopo kwa mujibu wa Qur'an na Sunna.

### 64. ITHIBATI YA KANUNI

Kanuni hizi zitatumika baada ya kupitishwa na kuthibitishwa na Halmashauri kuu ya BAKWATA Taifa.